**JINA:………………………………………………………………. NAMBARI:……………………**

**SAHIHI:…………………………………TAREHE:…………………………………………….**

**102/3**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 3**
**FASIHI**

# MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA MECS

**KIDATO CHA NNE**

**SEPTEMBA 2022**

**MUDA: SAA 2 ½**

***MAAGIZO:***

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
c) Jibu maswali **manne** pekee.
d) Swali la **kwanza** ni la **lazima.**
e) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki; yaani; Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Hadithi Fupi.
f) Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.
g) Majibu yote **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili
h) Karatasi hii ina kurasa **6** zilizopigwa chapwa
i) Watahiniwa ni **lazima** wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

more free exams at www.freekcsepastpapers.com

***<u>KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE.</u>***

| Swali | Upeo | Alama |
|---|---|---|
| 1 | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| | 20 | |
| Jumla | 80 | |

**1. <u>SEHEMU YA A: USHAIRI</u>**

**(SWALI LA LAZIMA)**

***Soma shairi hili kisha ujibu maswali yafuatayo.***

Nikumbuke mwanangu,
Kila asubuhi unapoamka
Kwenda kazini,
Unapochukua sabuni ya kunukia,
Na dodoki jororo.

Na kopo la koligeti,
Kwenda kukoga hamumuni,
Penye maji ya bomba,
Yaliyochujwa na kutakaswa,
Mororo…

Kumbuka nyakati zile,
Za staftahi ya sima na mtama,
Ndizi na nagwa,
Kwa mchicha na kisamvu,
Na ulipokwenda choo,
Ulilia kwa uchungu

Nikumbuke,
Unapotoka nyumbani asubuhi maridadi,
Katika suti ya moto,
Miwani ya pembe,
Viatu vya Parisi,
Saa ya dhahabu,
Unapong'oka kwenda kazini,
Katika Volvo,
Katika njia iliyosakafiwa

more free exams at www.freekcsepastpapers.com

Kumbuka,
Nyakati zile,
Mimi na mamako,
Tulinyojidamka,
Mara tu kwale wa kwanza,
Alipoanza kukoroma,
Jogoo wa kwanza hajawika,
Mimi nikachukua mundu na panga,
Mamako jembe na shoka,
Tukaelekea porini,
Kufyeka na kuchimbua

Nahubaki wajiandaa kwenda shule…
Nikumbuke,
Saa za jioni,
Unapovalia kitanashati.

more free exams at www.freekcsepastpapers.com

**Maswali**

(a)Thibitisha kuwa utungo huu ni shairi (alama 2)

(b)Fafanua toni ya utungo huu. (alama 1)

(c)Huku ukitoa mifano,linganua kati ya mistari toshelezi na mistari mishata. (alama 4)

(d) Eleza maudhui yoyote matatu yanayojitokeza kwenye shairi. (alama 3)

e) Kwa kutoa mifano tambua aina nne za taswira. (alama 4)

(f)Eleza mbinu za kimtindo zilizotumika katika shairi hili kando na taswira. (alama 4)

g)Tambua nafsi neni katika shairi hili na udhibitishe. (alama 2)

## SEHEMU B: RIWAYA

## Assumpta K. Matei - CHOZI LA HERI

***Jibu swali la 2 au 3***

**2.** "Sijui kama kijana umesoma ile nadharia ya "deconstruction". Ni muhimu pia ujue kwamba , ikiwa unataka kujiokoa au kuzoea hali mbaya inayokukabili, ni muhimu kujiingiza katika hali yenyewe, ukaikabili vilivyo ili uache kuiogopa , au iache kukuathiri vibaya.''

a) Eleza muktadha wa dondoo hili ( alama 4)

b) Tambua mbinu ya lugha iliyotumika kwenye dondoo. ( alama 1)

c) Eleza sifa **nne** za msemewa wa dondoo hili. ( alama 4)

d) Kwa kutolea mifano mwafaka riwayani, jadili nadharia ya 'Deconstruction' (alama 11)

**au**

**3.** Tathmini umuhimu wa usimulizi wa Pete katika kuijenga Riwaya Chozi la Heri. ( alama 20)

more free exams at www.freekcsepastpapers.com

## SEHEMU YA C : TAMTHILIA

## P. Kea - KIGOGO

***Jibu swali la 4 au 5***

**4**. Huku ukitoa mifano mwafaka, fafanua mbinu zinazotumiwa na utawala wa Majoka kuendeleza udhalimu katika jimbo la Sagamoyo. ( alama 20)

**au**

**5**. "… binadamu ni mavumbi na mavumbini aatarejea kwa maana, kwa tamaa mtu amependa kula kuku huku nduguze wakila kama kuku. Na katika uchu huo huo amependa kukifikia kilele cha ufanisi kwa kukanyaga migongo ya wenziwe. Hatajali kufanya ujahili uwao ule, hata kupora wafu, almradi tu aweze kulifikia dhamirio lake.''

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Eleza aina mbili za taswira zinazojitokeza katika dondoo. ( alama 4)

c) Tambua mbinu nyingine mbili za kimtindo katika dondoo hili. (alama 2)

d) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. ( alama 10)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI-TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

**6**. "Kwanza nilimwogopa sana…kwa sababu kila siku alinitishia…"

(a)Fafanua muktadha wa dondoo. (alama 4)

(b)Eleza sifa zozote nne za msemaji . (alama 4)

(c)Ni sababu zipi zilichangia msemaji kujikuta katika mikono ya mrejelewa? (alama 4)

(d)Jadili masaibu wanayopitia watoto huku ukirejelea hadithi hii (alama 8)

**au**

**S. Omar***: Shibe Inatumaliza*

**7** a).Jadili matumizi ya kinaya katika hadithi ya " Shibe inatumaliza'' (alama 10)

(b)"<u>Tunakula tu. Vyetu na vya wenzetu</u>… Na watakozaliwa miaka hamsini ijayo."
Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari kwa kutoa hoja kumi. (alama 10)

more free exams at www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

**8.** Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Malaika nakupenda Malaika
Malaika nakupenda Malaika
Nami nifanyeje?
Kijana mwenzio
Nashindwa na mali sina we!
Ningekuoa Malaika

Pesa zasumbua moyo wangu
Pesa zasumbua moyo wangu
Nami nifanyeje?
Kijana mwenzio
Nashindwa na mali sina wee
Ningekuoa Malaika

more free exams at www.freekcsepastpapers.com

**Maswali:**

a)Tambua utungo huu. (alama 1)

b)Thibitisha jibu la (a) . (alama 2)

c)Tambua nafsineni katika utungo huu. (alama 1)

d)Eleza toni inayojitokeza katika utungo huu. (alama 2)

e)Umealikwa kuwasilisha utungo huu mbele ya wanafunzi wa shule yako.Taja mambo sita utakayozingatia ili kufanikisha uwasilishaji huu. (alama 6)

f)Tambua na uthibitishe shughuli mbili za kijamii zinazojitokeza katika utungo. (alama 2)

g)Taja mbinu **mbili** za kimtindo zilizotumika katika utungo. (alama 2)

h)Eleza dhima ya utungo wa aina hii katika jamii. (alama 4)

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**